


JINSI YA KUTUMIA BAFU YA BLEACHI (EAU DE JAVEL KWA KIFARANSA)

Bafu za bleachi husaidia kupunguza idadi ya bakteria kwenye ngozi ili eczema isiambukizwe. Bafu za bleachi zinaweza kutumika kudhibiti eczema kwa watoto na watu wazima.

Utahitaji:

- Bafu la kuogea au bafu la mtoto
- Maji vuguvugu
- Ndoo (mbegeti) ya kaya ya lita 10
- Bleachi ya White King ya Kaya (nyumbani) isiyo na harufu - 12mL kwa lita 10 za maji
- Mafuta ya kuoga – vifuniko 1-2 kwa kila bafu ikipendekezwa
- Chumvi ya dimbwi (pool) au mezani – kikombe 1/3 kwa lita 10 za maji ikipendekezwa




Kabla ya kuanza, safisha na kausha mikono yako.



Jaza bafu kwa maji kwa kiwango kinachohitajika kwa ndoo ya lita 10 ili uweze kupima ni kiasi gani cha maji unachoongeza.

Dokezo

Unaweza kutaka kuashiria kiwango cha maji na alama ya kudumu au mkanda wa wambiso wenye nguvu ili uhitaji kupima mara moja tu.



Ongeza 12mL ya bleachi kwa kila ndoo ya lita 10 ya maji iliyomwagaji kwenye bafu (kwa nusu ya bafu ya familia nzima, ongeza 1/4 kikombe cha bleach). Ikipendekezwa ongeza chumvi na mafuta ya kuoga.




Ongeza 1/3 kikombe cha chumvi kwa kila ndoo ya lita 10 ya maji iliyotiwa ndani ya bafu.




Osha mtoto wako katika umwagaji ili kuhakikisha kuwa unalowesha uso na kichwa cha mtoto, uangalie usitiye maji machoni pa mtoto.




Ongeza vifuniko 1-2 vya mafuta ya kuoga.



Ikiwa mtoto wako ana vidonda vya eczema na ganda, safisha kwa upole maeneo haya ili kujaribu kuondoa ukoko.



Mara tu mtoto wako anapokuwa msafi, mtoe kwenye bafu ya bleach - usitumiye maji kuondoa bleach kwa mtoto wako baada ya kuoga. Kausha mtoto wako kwa kumpiga kwa upole na taalo.



Tumia steroid za kupakaa ku mwili na vinyweshaji unyevu kama ilivyoelekezwa na daktari au muuguzi wako.